


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



BUNGE LA TANZANIA

Mwongozo Kuhusu Hoja Binafsi Bungeni

Machi, 2018

Mwongozo Kuhusu Hoja Binafsi Bungeni



YALIYOMO

1. UTANGULIZI	1
1.1. Maana ya Hoja	1
1.2. Aina za Hoja	1
1.3. Maana ya Hoja Binafsi	3
1.4. Mantiki ya kuwa na Hoja Binafsi	3
2. UTARATIBU WA KUWASILISHA HOJA	4
2.1. Masharti ya Jumla	4
2.2. Fursa ya Mbunge kuwasilisha Hoja Binafsi	5
2.3. Taarifa ya Hoja	6
2.4. Hoja ambazo zinaweza kutolewa bila taarifa	7
2.5. Jinsi ya kuwasilisha Hoja Bungeni	7
2.6. Hoja ambazo haziwezi kutolewa	8
3. UTARATIBU WA KUJADILI HOJA	10
3.1. Kutoa Hoja	10
3.2. Hoja kuungwa Mkono	10
3.3. Kutenguka kwa Hoja	11
3.4. Hoja kujadiliwa	11
3.1. Kuhitimisha Hoja	11

4. MABADILIKO YA HOJA	12
5. KUONDOA HOJA	14
6. UAMUZI WA HOJA	14
7. UZOEFU WA BUNGE KATIKA KUSHUGHULIKIA HOJA BINAFSI	16
7.1. Hoja Binafsi ya Mhe. January Yusuf Makamba (Mb)	16
7.2. Hoja Binafsi ya Mhe. Halima James Mdee (Mb)	18
8. HITIMISHO	22
BIBLIOGRAFIA	24

1. UTANGULIZI

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 imetoa mamlaka kwa Bunge kutunga Kanuni za Kudumu kwa ajili ya kuweka utaratibu wa kutekeleza shughuli zake. Kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 89 (1) ya Katiba, Bunge limetunga Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 ambazo zinaweka utaratibu wa Waziri au Mbunge kutoa Hoja Bungeni.

1.1. Maana ya Hoja

Hoja ni suala lolote ambalo Waziri au Mbunge ataliwasilisha Bungeni ili liweze kupata uamuzi wa Bunge. Waziri au Mbunge anaweza kufanya hivyo kwa kutoa pendekezo kwamba suala hilo lijadiliwe Bungeni. Hoja yoyote inayopendekezwa kujadiliwa itazingatia masharti ya Katiba, Sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge, kama itakavyofafanuliwa katika mwongozo huu.

1.2. Aina za Hoja

Hoja mbalimbali zinaweza kupendekezwa kujadiliwa Bungeni kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Hoja hizo zinaweza kutolewa na Mawaziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamati za Bunge au Mbunge mwingine yeyote.

- (a) Mawaziri wanaweza kutoa hoja zifuatazo ili zijadiliwe Bungeni:-
- (i) Hoja ya kujadili utekelezaji wa Bajeti za kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa Bajeti;
 - (ii) Hoja ya kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa Serikali wa maendeleo wa muda mrefu au mfupi;
 - (iii) Hoja ya kutunga sheria pale ambapo utekelezaji unahitaji kuwapo sheria; na
 - (iv) Hoja ya kujadili na kuridhia Mikataba yote ya Kimataifa inayohusu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa.
- (b) Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaweza kutoa hoja ya kujadili na kupitisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali.
- (c) Kamati yoyote ya Bunge inaweza kutoa hoja ya kujadili Taarifa ya Kamati.
- (d) Mbunge mwingine yeyote anaweza kutoa hoja zifuatazo:-
- (i) Hoja ya kuahirisha Shughuli za Bunge zinazoendelea ili kujadili jambo la dharura;
 - (ii) Hoja ya kujadili jambo lolote linalohusu haki za Bunge; na

(iii)Hoja Binafsi kuhusu jambo lolote ambayo itatolewa kwa kuzingatia masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

1.3 Maana ya Hoja Binafsi

Hoja Binafsi ni hoja ya Mbunge asiyekuwa Waziri au Mwanasheria Mkuu wa Serikali anayoitoa ili ijadiliwe na kuamuliwa na Bunge. Baada ya hoja husika kujadiliwa, kuamuliwa na kuafikiwa, inakuwa Azimio la Bunge.

1.4 Mantiki ya kuwa na Hoja Binafsi

Uzoefu katika Mabunge mengi ya nchi za Jumuiya ya Madola unaonesha kuwa muda mwingi wa Bunge hutumika kutekeleza shughuli za Serikali, na hivyo kwa kiasi kikubwa kuwafanya Wabunge ambao ni wawakilishi wa wananchi kukosa muda wa kutosha kutoa hoja mbalimbali zinazohusu kero za wananchi wao.

Kwa kuzingatia hilo, Kanuni za Kudumu za Bunge zimeweka utaratibu kwa Wabunge kuleta Hoja Binafsi Bungeni, hususan pale linapojitokeza jambo lolote katika jamiu ambalo Serikali haijalifanyia kazi kwa wakati, na hivyo kuwa kero katika jamiu. Baada ya hoja husika kujadiliwa, Bunge linaweza kutoa maazimio ya kuitaka Serikali kushughulikia jambo hilo kama ilivyoamuliwa na Bunge.

2. UTARATIBU WA KUWASILISHA HOJA BINAFSI

Katika mpangilio wa Shughuli za Bunge, Hoja Binafsi za Wabunge ni kati ya shughuli zilizoordheshwa kutekelezwa na Bunge [Kanuni ya 30 (4) (n)].

Utaratibu wa Mbunge kuwasilisha Hoja Binafsi Bungeni umeainishwa katika Sehemu ya Nne ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Utaratibu huo umewekwa katika Kanuni ya 53 hadi ya 58 kuhusu hoja zinazoweza kutolewa Bungeni, uwasilishaji wa taarifa ya hoja, masharti ya uwasilishaji wa hoja, utaratibu wa kujadili hoja, mabadiliko ya hoja na jinsi ya kuondoa hoja Bungeni.

Mbunge anayetaka kuwasilisha Hoja Binafsi anaweza kuandaa hoja hiyo yeye binafsi, au akaandaliwa hoja hiyo na Ofisi ya Bunge ambayo imepewa mamlaka hayo kwa mujibu wa Kanuni ya 21 (1) (e) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

2.1 Masharti ya Jumla

Ili Mbunge aweze kuwasilisha Hoja Binafsi ni vyema akazingatia masharti mbalimbali yaliyowekwa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, ambayo baadhi yake ni yafuatayo:-

2.1.1. Kuwasilisha taarifa ya hoja(notice) kwa Katibu wa Bunge;

- 2.1.2 Taarifa ya hoja itolewe kwa maandishi na kuwekwa saini na Mbunge anayeitoa;
- 2.1.3. Taarifa ya hoja au hoja inayotolewa ili ijadiliwe isikiuke masharti ya Katiba, Sheria au Kanuni za Kudumu za Bunge; na
- 2.1.4. Isiwe hoja ambayo ina lengo la kutaka kujadili jambo ambalo lilikwisha amuliwa na Bunge katika kipindi cha miezi kumi na miwili iliyopita kabla ya kikao kinachoendelea.

2.2 Fursa ya Mbunge kuwasilisha Hoja Binafsi

Mbunge amepewa fursa ya kuwasilisha Hoja Binafsi ili ijadiliwe Bungeni, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Fasili ya (2) inaeleza kuwa:

“ Bila kuathiri masharti ya Katiba na Kanuni hizi, Waziri au Mbunge mwingine anaweza, kwa kutoa hoja, kupendekeza kwamba, suala lolote lijadiliwe Bungeni na hoja hiyo itaamuliwa kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hizi”.

2.3 Taarifa ya Hoja

- 2.3.1 Taarifa ya hoja itawasilishwa na kupokelewa na Katibu wa Bunge angalau siku moja ya kazi kabla ya Mkutano ambapo hoja hiyo inakusudiwa kuwasilishwa [Kanuni ya 55 (1)]. Hata hivyo, Spika anaweza kuruhusu hoja iwasilishwe Bungeni bila taarifa, kwa kutilia maanani udharura wa jambo lenyewe.
- 2.3.2 Taarifa ya hoja yoyote ni sharti itolewa kwa maandishi na kuwekwa saini na Mbunge anayeitoa kabla ya kupokelewa na Katibu [Kanuni ya 55 (2)].
- 2.3.3 Ingawa Kanuni za Bunge hazisemi kwamba taarifa ya hoja na maelezo ya hoja vitolewe kwa pamoja, lakini uzoefu unaonesha kuwa taarifa ya hoja na maelezo ya hoja vimekuwa vikiwasilishwa kwa pamoja. Maelezo hayo yanamwezesha Spika kuitafakari hoja husika ili aweze kutoa uamuzi kwa mujibu wa Kanuni. Taarifa ya hoja na maelezo ya hoja yakishapokelewa na kukubalika, hoja husika huwekwa katika Kitabu cha Shughuli za Mkutano wa Bunge kisha kwenye Orodha ya Shughuli za Kikao cha Bunge [Kanuni ya 55 (7)].

2.4 Hoja ambazo zinaweza kutolewa bila taarifa

Kwa mujibu wa Kanuni ya 55 (3) hoja zifuatazo zinaweza kutolewa bila taarifa:-

- 2.4.1. Kutengua Kanuni yoyote kati ya Kanuni za Bunge zinazotumika Bungeni;
- 2.4.2. Kuahirisha Bunge au kuahirisha mjadala;
- 2.4.3. Kutaka wageni waondoke Bungeni;
- 2.4.4. Kutaka ombi lililowasilishwa Bungeni lijadiliwe;
- 2.5.5. Kuahirisha Shughuli za Bunge zinazoendelea ili kujadili jambo la dharura;
- 2.5.6. Kuhusu jambo lolote linalohusiana na haki za Bunge; na
- 2.5.7. Kutaka Hati iliyowasilishwa Bungeni ijadiliwe.

2.5 Jinsi ya kuwasilisha Hoja Bungeni

Mbunge atawasilisha hoja yake Bungeni kwa kutoa maelezo pamoja na mapendekezo ili Bunge liweze kutoa uamuzi. Mfumo wa maneno ya hoja inayowasilishwa Bungeni utakuwa kama ifuatavyo:-

“ KWAKUWA ,

“NA KWAKUWA ,

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba ...”

2.6 Hoja ambazo haziwezi kutolewa

Spika anayo mamlaka ya kuikataa hoja yoyote inayokiuka masharti ya Katiba, Sheria au Kanuni za Kudumu za Bunge . Mfano, Spika hataruhusu hoja inayokiuka Ibara ya 99 ya Katiba, hususan masharti ya Ibara ndogo ya (2). Aidha, Spika hataruhusu hoja inayokiuka masharti ya Kanuni ya 95 ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Ibara ya 99 ya Katiba inaweka masharti yafuatayo:-

(1) Bunge halitashughulikia jambo lolote kati ya mambo yanayohusika na ibara hii isipokuwa kama Rais amependekeza kwamba jambo hilo lishughulikiwe na Bunge na pendekezo hilo la Rais liwe limewasilishwa kwenye Bunge na Waziri.

(2) Mambo yanayohusika na ibara hii ni haya yafuatayo:-

(a) Muswada wa Sheria kwa ajili ya jambo lolote kati ya mambo yafuatayo:-

(i) Kutoza kodi au kubadilisha kwa namna nyingine yoyote isipokuwa kupunguza;

- (ii) Kuagiza kwamba malipo au matumizi ya fedha yafanywe kutokana na Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali au mfuko wa Serikali mwingine wowote au kubadilisha kiwango hicho kwa namna nyingine yoyote isipokuwa kupunguza;
- (iii) Kuagiza kwamba malipo au matumizi ya fedha yafanywe kutokana na Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali au mfuko wa Serikali mwingine wowote wakati ikifahamika kwamba fedha iliyomo katika mifuko hiyo haikupangiwa itolewe kwa ajili ya malipo au matumizi hayo, au kuagiza kwamba malipo au matumizi yanayofanywa kutokana na mifuko hiyo yaongezwe;
- (iv) Kufuta au kusamehe deni lolote linalotakiwa lilipwe kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano;
- (b) Hoja au mabadiliko yoyote ya hoja kwa ajili ya jambo lolote kati ya mambo yaliyoelezwa katika aya ya (a) ya Ibara hii ndogo.

Hoja ikikataliwa, Katibu wa Bunge atairudisha hoja hiyo pamoja na vielelezo vyake vyote kwa Mbunge husika ikiwa imeambatana na maelezo ya sababu za kukataliwa kwa hoja hiyo chini ya [Kanuni ya 55(9)].

3. UTARATIBU WA KUJADILI HOJA

Utaratibu wa kujadili hoja yoyote ikiwa ni pamoja na Hoja Binafsi ya Mbunge upo kama ifuatavyo:-

3.1. Kutoa Hoja

Mbunge atakapoitwa na Spika kutoa hoja, atasimama mahali pake na kutoa hoja yake [Kanuni ya 56(1)].

3.2. Hoja kuungwa Mkono

Hoja hiyo itahitaji kuungwa mkono na Wabunge wasiopungua kumi na endapo hoja haitaungwa mkono itatenguka [Kanuni ya 56(2)]. Mbunge anayeunga mkono hoja atasimama tu mahali pake bila kusema lolote, kisha atakaa, lakini Mbunge aliyefanya hivyo bado atakuwa na haki ya kuizungumzia hoja hiyo hapo baadaye [Kanuni ya 56(3)].

3.3. Kutenguka kwa Hoja

Iwapo hoja imewekwa katika Orodha ya Shughuli za Bunge na Mbunge mtoa hoja anapoitwa na Spika anashindwa kuitoa, hoja hiyo itatenguka, isipokuwa kama kuna Mbunge mwingine aliyeidhinishwa na mtoa hoja, anaweza kuitoa kwa niaba yake [Kanuni ya 56(4)]. Hoja iliyotenguka yaweza kutolewa tena baadaye, baada ya mtoa hoja kutoa taarifa upya kwa mujibu wa Kanuni [Kanuni ya 56(6)].

3.4. Hoja kujadiliwa

Baada ya hoja kuungwa mkono itajadiliwa na Bunge na kuyakubali mapendekezo yaliyopo kwenye hoja, kuyaboresha au kuyakataa.

3.5. Kuhitimisha Hoja

Endapo hakuna Mbunge zaidi anayependa kuzungumzia hoja iliyotolewa, Spika atampa mtoa hoja nafasi ya kuhitimisha hoja yake [Kanuni ya 56(7)].

Mbunge mtoa hoja anaweza kuchukua nafasi hii kuwashukuru Wabunge wenzake kwa kumuunga mkono. Mwisho Mbunge atahitimisha kwa kusema, “Mheshimiwa Spika naomba kutoa hoja”.

4. MABADILIKO YA HOJA

4.1 Hoja ikishatolewa ili iamuliwe inaweza kubadilishwa kwa:-

(a) Kuondoa maneno fulani kwa ajili ya kuingiza maneno mengine;

(b) Kuondoa maneno fulani bila kuongeza mengine; na

(c) Kuingiza au kuongeza maneno mapya [Kanuni ya 57 (1)].

4.2 Mtoa hoja atamkabidhi Katibu wa Bunge maandishi yenye saini yake yanayoonyesha mabadiliko anayotaka yafanywe [Kanuni ya 57 (2)].

4.3 Kila badiliko linalopendekezwa sharti liwiane na hoja inayokusudiwa kufanyiwa mabadiliko [Kanuni ya 57 (3)].

4.4 Badiliko lolote halitaruhusiwa kama kwa maoni ya Spika, linapingana moja kwa moja na hoja ya msingi iliyotolewa [Kanuni ya 57 (4)].

4.5 Iwapo hoja ya mabadiliko inapendekeza kuondoa au kuingiza maneno mapya,

mjadala utahusu tu uondoaji au uingizaji wa maneno hayo [Kanuni ya 57 (5) & (6)].

4.6 Kama kuna hoja ya kufanya mabadiliko katika hoja ya awali ya mabadiliko, hoja hiyo ya pili itajadiliwa na kuamuliwa kwanza kabla ya ile hoja ya awali ya mabadiliko kufanyiwa uamuzi [Kanuni ya 57 (7)].

4.7 Mabadiliko ya hoja pia yanaweza kufanywa na Mbunge mwingine yeyote kwa kutoa hoja ya kufanya mabadiliko wakati wowote baada ya hoja anayotaka kuibadilisha kutolewa, lakini kabla Bunge halijahojiwa liifanyie uamuzi [Kanuni ya 58 (1)].

4.8 Endapo kuna mapendekezo mawili au zaidi ya kubadilisha hoja moja, Spika atawaita watoa hoja hizo kwa kufuata mpangilio atakaoamua. Baada ya mapendekezo yote mawili kuamuliwa, Spika ataitoa tena hoja ya awali ili ijadiliwe kama itakavyokuwa imebadilishwa [Kanuni ya 58 (2) & (3)].

5. KUONDOA HOJA

- 5.1 Hoja yoyote inaweza kuondolewa wakati wowote kabla hoja hiyo haijafikishwa Bungeni iwapo Mbunge mtoa hoja atatoa kwa Katibu, taarifa ya maandishi ya kuiondoa hoja hiyo [Kanuni ya 58 (4)].

- 5.2 Endapo hoja imefikishwa Bungeni, mtoa hoja anaweza tu kuiondoa hoja yake kwa kusimama mahali pake na kusema “Naomba ruhusa kuiondoa hoja”, na Spika ataliuliza Bunge kama linaafiki hoja hiyo kuondolewa. Ikiwa Wabunge walio wengi watakubali iondolewe, Spika atasema. “Hoja inaondolewa kwa idhini ya Bunge”, na hoja hiyo itakuwa imeondolewa, lakini iwapo hawatakubali, hoja hiyo itabaki [Kanuni ya 58 (5)].

6. UAMUZI WA HOJA

- 6.1 Kanuni ya 53 (2) inaelekeza kuwa hoja itaamuliwa kwa mujibu wa masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

- 6.2 Uamuzi wa Bunge hufanyika kwa kuzingatia

masharti ya Kanuni ya 79 kwa kufuata maoni ya Wabunge walio wengi waliohudhuria na kupiga kura Bungeni.

- 6.3 Fasili ya (3) inaeleza kuwa mjadala juu ya hoja unapomalizika, Spika atawahoji Wabunge ili kupata uamuzi juu ya hoja hiyo. Spika kwanza atataka uamuzi wa wale wanaoafiki kwa kusema: “wale wanaoafiki waseme ndiyo”. Na baadaye atataka uamuzi wa Wabunge wasioafiki kwa kusema: “wale wasioafiki waseme siyo”.
- 6.4 Uamuzi utapatikana kwa kufuata wingi wa sauti za Wabunge za Ndiyo au Siyo, na Spika atatangaza matokeo ya kura kwa kusema; “naamini walioafiki wameshinda” au “naamini wasioafiki wameshinda”.
- 6.5 Endapo kura za Ndiyo na Siyo zitalingana, Spika wakati akiwa amekalia Kiti atakuwa na kura ya uamuzi [Kanuni ya 79 (2)].
- 6.6 Baada ya uamuzi wa Bunge, mapendekezo katika hoja ya Mbunge kama yalivyofanyiwa mabadiliko au kama yatabaki kama yalivyoletwa na Mbunge yanakuwa Azimio la Bunge.

7. UZOEFU WA BUNGE KATIKA KUSHUGHULIKIA HOJA BINAFSI

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa nyakati tofauti lilipokea na kujadili Hoja Binafsi mbalimbali zilizowasilishwa na Wabunge. Baada ya kuzijadili, Bunge liliazimia kuitaka Serikali kutekeleza mambo mbalimbali yaliyoamuliwa na Bunge. Hapa chini ni baadhi ya Hoja Binafsi zilizojadiliwa na kuamuliwa na Bunge.

7.1 . Hoja Binafsi ya Mhe. January Yusuf Makamba (Mb)

Hoja Binafsi ya Mhe. January Yusuf Makamba (Mb) kuhusu Sheria ya Udhibiti wa Shughuli za Upangaji Nyumba za Makazi ilitolewa katika Mkutano wa Sita wa Bunge, Kikao cha Tisa cha tarehe 10 Februari, 2012. Rejea Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) uk. 77 hadi 95.

Hoja hiyo ilikuwa na mapendekezo yafuatayo:-

- (a) **KWA KUWA**, asilimia kubwa ya Watanzania, hasa waishio mijini, wanaishi kwenye nyumba za kupanga na karibu asilimia 40 ya kipato chao wanakitumia kwa ajili ya kulipia pango;
- (b) **NA KWA KUWA**, kumekuwa na

udhibiti mdogo wa biashara ya upangaji na kupelekea kuongezeka kwa vitendo vya unyanyasaji dhidi ya wapangaji, ikiwemo kudaiwa pango la miezi sita hadi mwaka mzima, tena kwa fedha za kigeni;

(c) NA KWA KUWA, kumekuwa na tatizo la makazi mijini na hivyo kuwalazimisha wapangaji kukubali masharti ya upangaji yanayokwenda kinyume na haki na kwa kuwa vitendo hivi vimekuwa vinaendelea kwa muda mrefu bila udhibiti;

(d) NA KWA KUWA, hakuna sheria mama inayodhibiti upangaji na inayolinda haki za mpangaji na kwa kuwa Sheria ya Ardhi ya 1999 na Sheria ya Mahakama ya Ardhi ya 2005 hazitoi udhibiti kamilifu wa sekta ya upangaji nyumba;

(e) KWA HIYO BASI, Bunge liazimie kuitaka Serikali, kwa haraka inavyowezekana, ilete Muswada wa Sheria ya Kudhibiti Shughuli za Upangaji wa Nyumba (Rental Housing Act) ambayo, pamoja na mambo mengine, itaweka utaratibu na udhibiti wa sekta ya upangaji wa nyumba ikiwemo kuweka haki na wajibu wa

wapangaji na wenye nyumba, kuweka mazingira ya ukuaji wa sekta ya makazi na kuanzishwa kwa Mamlaka ya Udhhibiti wa Sekta ya Nyumba (Real Estate Regulatory Authority).

- (a) Hoja Binafsi ya Mhe. January Yusuf Makamba (Mb) ilipitishwa na Bunge kwamba Serikali itaifanyia kazi kwa mujibu wa taratibu.

7.2. Hoja Binafsi ya Mhe. Halima James Mdee (Mb)

Hoja Binafsi ya Mhe. Halima James Mdee (Mb) kuhusu kuitaka Serikali kusitisha ugawaji wa ardhi hadi tathmini ya kina itakapofanyika kujua kiasi cha ardhi kilichopo mikononi mwa wageni. Hoja hii iliwasilishwa katika Mkutano wa Tisa, Kikao cha Nane cha tarehe 8 Novemba, 2012. Rejea Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) uk. 58 hadi 138.

Hoja ya Mhe. Halima James Mdee (Mb) ilikuwa na mapendekezo yafuatayo:-

- (a) **KWA KUWA** rasilimali ardhi ndiyo urithi pekee wa asili wa Tanzania kwa Mtanzania katika kujitafutia riziki na kuendelea na maisha yake;
- (b) **NA KWA KUWA** idadi ya watu inaongezeka wakati ukubwa wa

ardhi hauongezeki jambo ambalo linaoonyesha dhahiri kwamba kuna hatari ya kiasi cha ardhi kilichopo kisisosheleze mahitaji halisi ya wananchi;

- (c) **NA KWA KUWA** imebainika kwamba uwekezaji wa ardhi unaofanywa na Makampuni ya nje haujawasaidia wananchi kwa maana ya fursa za ajira na upatikanaji wa chakula kwa kiwango kilichoahidiwa na Serikali na Makampuni hayo;
- (d) **NA KWA KUWA** ugawaji huu wa ardhi kwa wawekezaji unakwenda sambamba na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu ikiwa ni pamoja na wananchi waliokuwa katika maeneno hayo kupigwa, kuvunjiwa nyumba zao na kufukuzwa bila kulipwa fidia;
- (e) **NA KWA KUWA** kwa kiasi kikubwa zoezi la ugawaji wa ardhi kwa wawekezaji linakiuka sheria za nchi ambazo zinataka wananchi waarifiwe mapema juu ya ugawaji huo wa ardhi na kushirikishwa kikamilifu ili waweze kufanya maamuzi sahihi kwa maendeleo yao, jambo ambalo halifanyiki;

- (f) **NA KWA KUWA** mikataba ya ugawaji wa ardhi inafanyika kwa usiri mkubwa sana, jambo ambalo linaashiria mazingira ya rushwa na kutia shaka kama maslahi ya nchi yanazingatiwa;
- (g) **NA KWA KUWA** Serikali inapata kodi kidogo sana kutokana na uwekezaji katika ardhi, yaani sh. 200/= kwa hekta kwa mwaka na ikizingatiwa muda wa kukodisha ardhi kisheria ni miaka 99;
- (h) **NA KWA KUWA** asilimia 80 ya Watanzania wanategemea ajira katika Sekta ya Kilimo ambacho msingi wake ni ardhi;
- (i) **NA KWA KUWA** , Ibara ya 63 (2) (c) na (d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inasema kwamba: “Kwa madhumuni ya utekelezaji wa madaraka yake, Bunge laweza kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu na muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano na kutunga Sheria ya kusimamia mpango huo na kutunga sheria pale ambapo utekelezaji unahitaji kuwepo kwa Sheria”;

(j) **KWA HIYO BASI**, naliomba Bunge lako Tukufu liazimie kwamba zoezi la ugawaji wa ardhi kwa wawekezaji wa nje na ndani, lisitishwe hadi hapo tathmini ya kina itakapofanyika kubaini ni kiasi gani cha ardhi kipo mikononi mwa wawekezaji na wasio wawekezaji na kwamba tathmini ya kina ifanyike ili kuweza kubaini raia wa kigeni na wa ndani waliojipatia ardhi kinyemela kupitia Serikali za Vijiji kinyume na matakwa ya Sheria za Ardhi Na. 4 na Na. 5.

Hoja ilijadiliwa na baada ya kufanyiwa mabadiliko, Bunge liliazimia kama ifuatavyo:-

Zoezi la ugawaji wa ardhi kwa wawekezaji wa nje na wa ndani lifanyiwe tathmini ya kina ili kubaini ni kiasi gani cha ardhi kipo mikononi mwa wawekezaji na wasio wawekezaji;

Tathmini itakayofanyika ibaini raia wa kigeni na wa ndani waliojipatia ardhi kinyemela kupitia Serikali za vijiji kinyume na matakwa ya Sheria ya Ardhi, Na. 5 ya mwaka 1999 na taarifa ya tathmini hiyo italetwa katika Bunge la mwezi Aprili, 2013.’

8. HITIMISHO


Hoja Binafsi ya Mbunge kama ilivyofafanuliwa katika Mwongozo huu, ni nyenzo muhimu sana kwa Wabunge kuwajibika kwa wapiga kura wao. Aidha, Hoja Binafsi ya Mbunge ni njia anayoweza kuitumia Mbunge kuisimamia Serikali kwa niaba ya wananchi ili iwajibike kutatua kero zao.

Hivyo, Wabunge wanashauriwa kuitumia fursa ya Hoja Binafsi ipasavyo.

Hata hivyo, ili Hoja Binafsi ya Mbunge iweze kuamuliwa na kuafikiwa na Bunge, lazima iandaliwe na kuwasilishwa kwa kuzingatia masharti ya Katiba, Sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge kama yalivyofafanuliwa katika Mwongozo huu.

BIBLIOGRAFIA

- Erskine **May** (2011),
Parliamentary Practice (24th Edition), Lexis Nexis
- **Kanuni za Kudumu za Bunge**, Toleo la Januari, **2016**
- Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka **1977**
- M. N. **Kaul** and S. L. **Shakdher** with G. C. Malhotra- Editor **(2001)**,
Practice and Procedure of Parliament (5th Edition), Lok Sabha Secretariat, Metropolitan Book CO. PVT. LTD
- M. N. **Kaul** and S. L. **Shakdher** with P. D. T. **Achary** - Editor **(2009)**,
Practice and Procedure of Parliament (6th Edition), Lok Sabha Secretariat, Metropolitan Book CO. PVT. LTD
- Taarifa Rasmi za **Bunge (Hansard)**,
Mkutano wa Sita, Kikao cha Nane- Tarehe 8 Februari, 2017
- Taarifa Rasmi za **Bunge (Hansard)**,
Mkutano wa Tisa, Kikao cha Nane- Tarehe 8 Novemba, 2012
- Taarifa Rasmi za **Bunge (Hansard)**
Mkutano wa Tisa, Kikao cha Tisa – tarehe 9 Novemba, 2012
- **The House of Representative (2014)**
Guide to Procedure (5th Edition), Department of the House of Representative, Canberra





Mwongozo huu umeandaliwa na
Ofisi yaBunge
S.LP 941
Dodoma

